TANGAZO LA SERIKALI Na. 321 ...la tarehe... 30/9/2011

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA 290

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA STENDI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI, 2010

Jina na mwanzo wa kutumika	1	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Stendi) za Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.
Eneo la matumizi		Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji
Tafsiri	3	Katika Sheria Ndogo hizi isipokua itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yoyote wa Halmashauri aliyeidhinishwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Basi" maana yake ni Gari lolote lililosajiliwa na linalosafirisha Abiria na mali zao na liendalo nje ya Manispaa au Ndani ya Manispaa.

"Basi dogo" maana yake ni basi dogo lolote lililosajiliwa kusafirisha Abiria ndani na nje ya Himaya ya Halmashauri.

"Gari" maana yake ni Gari lolote linalofanya biashara na itajumiusha basi lolote la abiria, Lori, Teksi au Pick-Up au gari lolote la Biashara.

"Gari la Binafsi" maana yake ni gari lolote la mtu au kampuni binafsi ambalo halifanyi biashara.

"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji.

"Kituo" maana yake ni eneo lolote lililoteuliwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuegesha magari ya Biashara.

"Lori" maana yake ni Gari lolote kubwa lililosajiliwa na kufanya shughuli za biashara katika kuegeshwa eneo lolote ndani ya Himaya ya Halmashauri.

"Maegesho binafsi" maana yake ni maegesho yoyote yatakayowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuegeshea magari binafsi kwa muda utakaoonyeshwa katika Sheria Ndogo hizi.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Pick-Up" maana yake ni gari dogo la wazi lililosajiliwa na kufanya Biashara ya kubeba mizigo.

"Teksi" maana yake ni gari lolote dogo lililosajiliwa kwa madhumuni ya kubeba abiria.

"Ushuru" maana yake ni kiwango cha fedha kilichopangwa na Halmashauri kitakacholipwa na mmiliki wa Gari litakapoingia au kuegeshwa Kituoni.

Ushuru

4 (1) Halmashauri inaanzisha na kutoza ushuru wa stendi kwa kila gari kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa Gari la biashara kuhakikisha kuwa analipa ushuru kila akapoingia au kuegesha katika kituo maalum kilichotengwa na Halmashauri.

(3) Ushuru huo utatozwa gari litakapoingia, kutoka au kuegeshwa katika kituo kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(4) Ushuru wa stendi utalipwa kwa Afisa Muidhiniwa au Wakala ambaye atatoa Stakabadhi itakayolingana na fedha iliyolipwa.

Maegesho ya magari binafsi

5 (1) Halmashauri itatenga maeneo maalum kwaajili ya maegesho ya magari binafsi au ya biashara wakati mwenye gari au abiria akipata huduma sehemu nyingine.

(2) Gari lolote litakaloegeshwa katika eneo hilo litalipiwa ushuru kwa viwango vilivyoonyeshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi

(3) Endapo kuna mtu yeyote atataka sehemu maalum kwaajili ya kuegesha gari lake binafsi atalipia ushuru na Halmashauri itaweka alama kuonyesha kuwa sehemu hiyo imelipiwa na mtu binafsi (Private Parking)

(4) Halmashauri itatoza ushuru magari yote yatakayoegeshwa kwenye eneo la hifadhi ya barabara. (Road reserve)

Halmashauri kukamata gari

6 (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukamata gari lolote ambalo halijalipiwa ushuru na kulipeleka katika yadi ya Halmashauri mpaka hapo mmiliki wake atakapolipa kiasi cha ushuru unaodaiwa.

(2) Halmashauri haitahusika wala kuwajibika na uharibifu wowote utakaotokea;-

(a) wakati wa kukamata, kuvutwa, au kukokotwa gari hilo kulipeleka kwenye yadi ya Halmashauri.

(b) kwa kipindi chote gari litakapokuwa katika yadi ya Halmashauri.

(2) Gari lolote litakalokamatwa na kutunzwa katika yadi ya Halmashauri litalipiwa kiasi cha Shilingi Laki Moja (100,000/=) kila siku mpaka siku mmiliki wake atakapolipa ushuru anaodaiwa pamoja na gharama ya kutunza gari hilo.

Halmashauri kuendesha msako

7 Halmashauri kwa kushirikiana na Askari wa Kikosi cha usalama barabarani au Askari yoyote anayetambulika na Serikali itaendesha msako wa kukamata magari yoyote yasiyolipiwa ushuru.

Makosa

8 Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yoyote:-

(i) atakataa, kukwepa, au kushindwa kulipa ushuru

(ii) ataosha gari au kufanya matengenezo makubwa ndani ya stendi

(iii) atasababisha au kufanya fujo katika eneo la stendi

(iv) atakwamisha au kuchochea juu ya ushuru au utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

(v) atapakia abiria nje ya vituo vilivyoruhusiwa.

(vi) ataegesha au kulaza Gari katika barabara za Halmashauri.

(vii) atamzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake

Adhabu

9 Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi 50,000/= au kifungo cha miezi 12 jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufilisha kosa 10 Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote atakaekwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa ushuru anaodaiwa pamoja na faini isipokuwa faini hiyo haitazidi kiwango kilichoainishwa katika kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI

USHURU WA STENDI

Na	AINA YA GARI	USHURU
1.	Mabasi makubwa	1,000/= kwa siku
2.	Mabasi madogo	1,000/= kwa siku
3.	Malori	1,000/= kwa siku
4.	Pick-up	1,000/= kwa siku
5.	Taxi	1,000/= kwa siku

JEDWALI LA PILI

USHURU WA MAEGESHO

NA	AINA YA GARI	KIASI KWA SAA	
1.	Gari dogo binafsi au biashara	200/= kwa dakika moja hadi saa moja	2,000/= kwa siku
2.	Gari la kati la Binafsi au biashara	300/= kuanzia dakika moja hadi saa moja	3,000/= kwa siku
3.	Gari kubwa la Binafsi au biashara	400/= kuanzia dakika moja mpaka saa moja	10,000/= kwa siku
4.	Gari lolote la egesho binafsi		100,000/= kwa mwezi

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji unabandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 31 Julai, 2009
Nembo hiyo umebandikwa mbele ya

LEWIS. K. KALINJUNA
Mkurugenzi
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

SHABANI MAMBO
Naibu Mstahiki Meya
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

NAKUBALI **MHE. MIZENGO. P. PINDA**
WAZIRI MKUU

DODOMA..2.9/7/2011..